HISTORIA YA MKOA MJINI MAGHARIBI

Kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 Zanzibar iligaiwa jiografia katika maeneo makubwa matatu yaliyopewa hadhi ya Wilaya ambayo ni :-

- Wilaya ya Mjini
- Wilaya ya Mashamba
- Na Wilaya ya Pemba

Kutokana na hali hiyo Zanzibar baada ya Mapinduzi ikayapa maeneo hayo hadhi ya kuwa Mikoa, hivo kuifanya Zanzibar kugawika katika Mikoa mitatu, Mikoa miwili Unguja na mmoja Pemba. Pia Zanzibar iligaiwa katika *mudiriat* 10 ambapo kwa Unguja 06 na Pemba 04, kwa wakati huo eneo la Mkoa mjini mMagharibi likijuulikana kwa jina la Mkoa Mjini ambao umegaiwa katika *mudiriat* ya Mjini na mudiriat ya shamba, baadae *mudiriat z*ikaitwa Wilaya na viongozi waliitwa Wakuu wa Wilaya (*Area Commission*) .
Katika miaka ya 1970, Zanzibar iligaiwa katika Mikoa 04 *ikijumuisha:-*

- Mkoa Mjini Magharibi
- Mkoa wa Kusini
- Mkoa wa Kaskazini
- Mkoa wa Pemba

Ambapo Mkoa Mjini Magharibi uligaiwa katika Wilaya ya Mjini na Magharibi. Mikoa yote ya Zanzibar ukiwemo Mkoa Mjini Magharibi ilikuwa chini ya Ofisi ya Rais, kuanzia wakati wa Mapinduzi hadi ilipoanzishwa Ofisi ya Waziri |Kiongozi kwa toleo la tarhe 03 May 1984 la mabadiliko ya Wizara na Idara zake. Ofisi za Mikoa ukiwemo Mkoa Mjini Magharibi miaka ya 2000 wakati wa utawala wa Rais w awamu ya tano Dk Salmin Amour Juma zilikuwa chini ya wizara yta Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ hadi mwaka 2010 zilipopelekwa chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katika kipindi cha mwaka 1980 Mkoa Mjini Magharibi ulikuwa na majimbo 13, ambapo majimbo 11 ya Wilaya ya Mjini na Majimbo 2 ya Wilaya ya Magharibi. Majimbo hayo yalikuwa yakiongozwa na wenye viti wa tawi la CCM wakati chama kiliposhika hatam kwa mfumo wa chama kimoja, ambao ni watendaji waliowakilisha

Serikali hadi mwaka 1986 ulipoanzishwa mfumo wa kutenganisha uongozi wa chama na Serikali kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Mabadiliko makubwa Zaidi ya kutengenishwa Chama na Serikali yalitokea Juni 1992 ulipoanzishwa mfumo wa vyama vingi. Baada ya Mapinduzi ya 1964 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi ilikuwa ikitumia jengo linalotumiwa na ZBC TV hivi sasa (Karume House) ambalo kabla ya Mapinduzi lilijuulikana kwa jina la Khalifa Holl katika miaka ya70, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi lilikuwa likitumia jengo la *Majestic cinema* na baadae Ofisi ya Mkoa na Wilaya ya Mjini ikahamia jengo la Manispaa (Baharmal building) na baadae ilihamia jengo la Sanaa na Utamaduni Forodhani na katika mwaka 1991 Ofisi ilihamia Vuga hadi hii leo. Wakuu wa Mikoa waliongoza Mkoa Mjini Magharibi na mwaka

Nam	**Jina la Kiongozi**	**Mwaka alioanza**	**Mwaka aliomaliza**
1	Bw: Ali Mwinyi Gogo	1964	1965
2	Bw: Mdungi Usi	1965	–
3	Bw: Tawakal Khamis	–	1969
4	Bw: Saidi Washoto	1969	1983
5	Bw: Tahir Silima	1983	1985
6	Bw: Rajab Kheir Yussuf	1985	1985
7	Bw: Ame Mohamed	1985	–
8	Bw: Ramadhan Said	–	–
9	Dk: Ishau Abdallah Khamis	1990	1991
10	Bw: Salum Juma Othman	1991	1995
11	Bw: Abdulla Rashid	1995	1998

12	Bw:Muhsin Ameir	1998	2001
13	Bw: Abdulla Mwinyi Khamis	2001	2017
14	Bw: Ayoub Mohammed Mahmoud	2017	2019
15	Bw: Hassan Khatib Hassan	2019	Hadi sasa